manihaji

بسم الله الرحمن الرحيم

26/Safar/1427H=26March/2006 AD.Madinatul Rasuul s.a.w.-Saudi Arabia.
Makala namba 6.

# HII NDIYO DAAWA YETU

## JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIH

## UHARAMU WA KUYAJENGEA MAKABURI

Amesema Swahaba mtukufu Jabir bin Abdillahi r.a;
[Amekataza Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w
kulipaka chokaa kaburi,na kulikalia**,na kulijengea** ].
Tazama sahihi muslim juzuu 3ukurasa62.

MUANDISHI;

ABUL FADHLI QASSIM MAFUTA QASSIM.

بسم الله الرحمن الرحيم

Ewe mola wetu ni zako wewe sifa njema zote,na shukrani zote,
ni zako wewe sifa njema vile zinavyo lingana na utukufu wako,na ukubwa wako,ni zako wewe sifa njema mpaka uridhike,na pale unaporidhika, na baada ya kuridhika.

Na sala na salamu zimfikie kipenzi chetu,Mtume wetu Muhammad, na jamaa zake,na maswahaba zake wote,na walioiandama njia yao kwa wema mpaka siku ya malipo.
Ndugu muislamu!
Katika sehemu hii ya pili ya mfululizo wa makala zetu UHARAMU WA KUYAJENGEA MAKABURI. Tutazijadili hoja na dalili zilizotumika katika kulitetea jambo hili la haramu .

Vijana hao wa Msikiti wa Buguruni kwa Mnyamani walifanya jaribio la kutaka kuzipindisha dalili za kisheria ili kutumukia mradi wao.
Na hapa tunaendelea kuzinyambuanyambua hizo hoja zao kwa ufupi na majibu yake ya kielimu pamoja na kubainisha makosa ya kielimu;

**Kosa lake la kumi;**
Amemtaja Imamu Ibin Juraij mara kumi kimakosa kwa kumuita Ibin Juraih.
**Jawabu yetu;**

Na sawasawa ni Ibin Juraij,na haiwezikani likawa hili ni kosa la kiuandishi,vipi unakosea mara kumi wala hugutuki!

Naam,kwa mtu msomi kutomjua Imamu huyu ni kosa,hasa unapokuwa unalizungumzia suala la elimu ya hadithi.

Na hili ni miongoni mwa makosa yanayo dhihirisha kiwango duni cha elimu ya muandishi,na kuwa yeye hastahiki kuwa msemaji wa waislamu,anatakikana kwanza ataalamike.

**Kosa lake la kumi na moja;**
Katika ukarasa wa 3 mstari wa nane kutoka chini amesema hivi;
[katika hadithi hizo kuna majina ya watu wawili ambao hawafai kwanza yumo mtu aitwa WAHAB na ya pili kuna huyu aitwaye luhay'ah tukianza na hadith ya kwanza inatupwa nje kwa kuwemo huyu WAHAB kwani majina ya wahab wako wengi sana na sasa

huyu WAHAB aliyehapa hali yake haitambuliki hata kidogo kwani kuna majina ya WAHAB zaidi ya kumi na saba sasa ni yupi na wengi wao ni wazushi.].

**Jawabu yetu;**

Kwanza kabisa,tunakuomba samahani ndugu msomaji kwa kukunukulia vichekesho hivi,na kusema kama alivyosema mshairi;

أوردها سعد وسعد مشتمل
ما هكذا تورد يا سعد الابل

Pili ni kuhusu maneno yake tuliyo yapigia mistari,yote hayo ameyataja kimakosa,jina lililo kuja katika is'nadi ya hadithi aliyoitaja si WAHAB sawa sawa ni WUHAYBU.
Nahuyo ni Wuhaybu bin Amri bin Uth'man An Namary (1)

Ama madai yake ya kwamba hadithi itupwe nje kwasababu eti Wahab wako wengi zaidi ya kumi na saba,
na huyu hajulikani ninani,hivi ni vituko vya aakhiriz zaaman.

Kwasababu yeye anakosea kuyataja majina ya maulamaa kisha anasema kuwa hawajulikani !
Sasa huyo tumekutajia na hata ukiirejea Sunan Ibni majah,na ukaitazama sanad ya hadithi hiyo namba 1564.utakuta amelitaja jina la Wuhaybu na si Wahab kama anavyodai sheikh wetu wa Buguruni .

kwahiyo madai ya kwamba hadithi itupwe nje kwasababu tu haiwafikiani na matamanio yake,na kwasababu ya uchache wake wa elimu,huko ni kutoziheshimu hadithi sahihi za Bwana Mtume s.a.w.
Kwahiyo tunasema kwamba;

Hadithi hii haitotupwa nje,bali yeye ndiye wa kutupwa nje ya uwanja wa elimu.
Ama neno alililoliandika luhay'ah ni kosa na sawa sawa ni Ibin Lahia'a.
Ama kuhusu huyu Ibin Lahia'a ni kweli ni dhaifu,ila wakipokea kutoka kwake baadhi ya wapokezi,kama wale wanaoitwa Abaadila (Abdullahi bin mubarak,Abdullahi bin Wahab,Abdullahi bin Yazid al muq'ri,Abdullahi bin Qa'anabi al Qa'anaby) na Qutayba bin Said hadithi zao kutoka kwake ni sahihi.

Amakuhusu hadithi hiyo aliyoipokea Ibin Lahia'a imekuja kwa njia nyingine isiyokuwa ya Ibin Lahia'a kutoka kwa Jabir{r.a.} amesema;

[amekataza Mtume{s.a.w.} kulipaka chokaa kaburi na kulikalia na kulijengea ..].

Na hadithi hii ni sahihi ameipokea Imamu muslim,Abu Daud, Tir'midhy, An nasai,Al Hakim,na Al bayhaqi.

Swali ;
kwanini mpaka ukaitafute hadithi ya Ibin Lahia'a,na hali hadithi sahihi ipo? Au hujui kuzitafuta hadithi?

**ان كنت لا تدري فتلك مصيبة**
**وان كنت تدري فالمصيبة أعظم**

## Kosa lake la kumi na mbili;

Sheikh amemtaja Sayyid'na Muhammad Rasuulullahi {s.a.w.} takribani mara saba kwenye makala yake,lakini hakumswalia hata mara moja japo kwa ishara ya{s.a.w.} basi yako wapi mapenzi kwa mtukufu huyu ! au kumswalia mpaka kwenye hadhara za maulidi?

Katika ishara za mapenzi ya kweli juu ya mjumbe huyu mtukufu{s.a.w.} ni kufuata Sunna zake,na kuacha aliyo yakataza kama kujengea makaburi n.k,na kukithirisha kumswalia kila anapotajwa {s.a.w.}.

## Kosa lake la kumi na tatu;

Amesema katika ukurasa wa mwisho katika mstari wa 1-3;

[nadhani mmeona mpaka hapo hayo maegemeo yenu yote yana mushkheli mkubwa basi ni kwanini mwawa viziwi namna hiyo kiasi cha kufikia kukufurisha waislamu wenzenu kwa kutegemea hadith dhaifu kama hizi..].

## jawabu yetu;

1- Bila shaka ndugu muislamu kwa ufafanuzi tulio utoa umefahaamu kwamba maegemeo yetu juu ya kaharamisha

kujengea makaburi,na kuyavunja iwapo watu watahalifu wakayajengea hayo makaburi.

Umefahamu kuwa hoja hizo hazina mush'keli wowote,bali umegundua kwamba mush'keli uko kwa sheikh wa msikiti wa kwa mnyamani ana matatizo katika kuyafahamu maneno ya maulamaa,na ni bingwa wa kupindisha makusudio ya ibara za maulamaa hao !

2-Ama kusema kwamba sisi ni viziwi,ni kweli sisi ni viziwi mbele ya kauli ya Mwenyezi Mungu{s.w.t.} na Mtume wake {s.a.w.} hatusikii kauli ya yoyote yule iliyo kinyume na kauli zao, hivi jamani kiziwi ni yule anaye ihalifu kauli ya Allah na Mtume wake {s.a.w.} anaposema;

Usijengee kaburi yeye analijengea?

Au ni yule anayetii kauli hiyo na kuwaita waislamu wengine kwenye kutii?

Lakini siku zote watu wasio na hoja na dalili,kutukana watu ndio kazi yao.

3-Kudai kwamba sisi tunawakufurisha waislamu wenzetu kwasababu ya kutegemea hadithi hizi dhaifu,ni madai yasiyo na dalili yoyote,amesema al Buswiry katika hamziya yake;

والدعاوى ما لم تقيموا عليها بينات أبناؤها أدعياء

Sisi tuna mkufurisha yule anaye kufurishwa na Allah{s.w.t} na Mtume wake{s.a.w.} pamoja na kuchunga vigezo vya kumkufurisha.
Na pia usije ukadhani kwamba uislamu ni kama kabila haubanduki vyovyote utakavyo fanya basi wewe ni isilamu tu!
La, uislamu una mipaka yake na haya tuna kubaliana waislamu wote ni ipi ? hapo ndipo kwenye makindano baina yetu na haya tutayaeleza kwa kina katika makala yetu,ni mawahabi au ah'lus sunna, tafadhali usiikose.

Na kwa ufanunuzi tulio utoa tumethibitisha kwamba hadithi tunazo zitegemea si dhaifu,bali sheikh wetu ndiye aliye na udhaifu wa kuelewa makusudio ya Ulamaa, na kama hivyo anavyosema ni kweli, basi pale ikimjia hamu ya kutaka kujitetea atutajie hao

maulamaa walio zidhoofisha hadithi hizi,na hii ni challenge tunaitoa kwa mtu yoyote yule anae mudu kufanya hivyo kielimu.

**Kosa lake la kumi na nne;**

Ni pale aliposema katika ukurasa wa mwisho mstari namba 6-14; [ tunawauliza ndugu zetu nyinyi wa Answar huu ufalme wa Saudia mnaoukumbatia je uko katika Tawhiid maana ufalme nao ni katika shirki.. ].!

**Jawabu yetu;**

Kwanza kabisa ndugu yangu muislamu nataka ufahamu kwamba hapa siko katika kuutetea ufalme na wafalme wa nchi yoyote ile.

Bali niko katika kuifanyia kazi aya ya152 ya suratul al an'am aliposema Allah {s.w.t.};

وَإِذَا قُلْتُمْ فَاعْدِلُواْ

[…na mnaposema semeni kwa uadilifu…].al An'am 152.

Na hakuna uadilifu kama sheria ya kiislamu,sasa basi tunamuomba ndugu yetu sheikh wa msikiti wa kwa mnyamani atujibu maswali haya yafuatayo maana elimu ni bahari;

Hivi haya uliyo yasema kwamba ufalme ni shirki ni maoni binfsi au ni ndiyo sheria ya kiislamu?

Kama ni maoni binfsi mbona umeyapa hukumu ya kiislamu?Au hujui kwamba hakuna rai katika hukumu za kislamu,ila zitakapokuwa rai hizo zimeegemea kwenye dalili za kisheria?

3-Na kama hiyo ni hukumu ya kisheria ya kiislamu, tafadhali tunaomba -hasa mimi binafsi -unielekeze ni aya gani au hadithi gani au ni mwanawachuoni gani katika wanawachuoni wa kubwa tena wakutegemewa aliye lizungumzia suala hili na kulipa hukumu kama hiyo uliyo itoa wewe,kwa ufupi ninani aliye kutangulia katika kutoa hukumu hii?

Kitabu gani ukurasa wangapi?Tafadhali nijibu kielimu.

4-Je unaijua historia sahihi ya ufalme katika umma huu wa Muhammad {s.a.w.} ?

Na je unamjua mfalme wakwanza katika umma huu? je unasemaje kuhusu yeye mwenyewe na ufalme wake? Je na Mtume {s.a.w.} naye alisemaje kuhusu yeye na ufalme wake?

5- unasemaje kuhusu hii hadithi sahihi ya Mtume {s.a.w.} aliposema;

".ثم ملك بعد ذلك,الخلافة فى أمتي ثلاثون سنة"
[ukhalifa katika umma wangu ni miaka thelathini,kisha ni ufalme baada ya hapo ]?
Angalia jamiit tir'midhy hadithi namba2226.

6-ikiwa ufalme ni shirki kama unavyodai, sijui unasemaje kuhusu pale aliposema Allah {s.w} ;

**251البقرة} ...وَقَتَلَ دَاوُودُ جَالُوتَ وَآتَاهُ اللّهُ الْمُلْكَ وَالْحِكْمَةَ {**

[..na Daudi akamwua Jaluti,na mwenyezi mungu akampa (Daudi) Ufalme,na hikima(utume)..].
Al Baqara Aya 251.

7-Je unasemaje pale Nabii Suleiman bin Daudi alipomwambia mwenyezi mungu;
**35ص} ...قَالَ رَبِّ اغْفِرْ لِي وَهَبْ لِي مُلْكاً {**

[Akasema:Ee mola wangu!nisamehe na unipe Ufalme…].
Surat Swaad Aya ya 35.

8-Je utajibu nini pale Nabii Mussa alipowakumbusha wana wa Israeli neema walizo neemeshwa na mwenyezi mungu, akawaambia;

**وَإِذْ قَالَ مُوسَى لِقَوْمِهِ يَا قَوْمِ اذْكُرُواْ نِعْمَةَ اللّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَعَلَ فِيكُمْ أَنبِيَاء وَجَعَلَكُم مُّلُوكاً {**
**20المائدة }**
[…Enyi watu wangu! kumbukeni neema za mwenyezi mungu zilizo juu yenu, Alipowafanya manabii miongoni mwenu,na akakufanyeni wafalme...].

**kosa lake la kumi na tano;**

Amesema sheikh huyo wa Buguruni,tena kwa hamasa kabisa,anaonekana kwamba ni mwana harakati mzuri aliye na hamasa bila elimu;

[..hata hao masheikh wenu wa Saudia mliokuwa mkiwategemea akina  Muhammad bin Abdul Wahab yeye si ndiye alishiriki kusimika ufalme na mpaka leo hii mtu hawezi kuwa mufti ndani ya saudia mpaka atoke katika familia yake yeye je hiyo kweli ni sunna mbona mko kimya hamkemei ukafiri huu na shirki hii ya ufalme ..]

**Jawabu yetu;**

Ama madai ya kwamba Saudia mtu hawezi kuwa mufti mpaka atoke ndani ya familia ya Sheikh Muhammad bin Abdil Wahab, suala hili tunalijibu kwa swali hili;

Utajibu nini ukiulizwa kuhusu al allaamah Ibnu Baazi {r.a.t.} ambaye alikuwa ni muf'ti wa Saudia kabla ya muti huyu wa sasa, naye hatoki ndani ya familia ya Muhammad bin Abdil Wahab?

Je huoni kwamba unasema urongo? Au umesahau? basi unapokuwa mrongo kuwa mwepesi wa kukumbuka.
Au hilo hulijui?
Basi kwanini usimame kushupalia jambo usilo na ujuzi nalo? Je kufanya hivyo ni uadilifu? Basi sheikh muogope mola wako.

Ndugu waislamu tuweni waadlifu tunapo wahukumu watu na chuki zetu zisituzuie kuwafanyia watu uadilifu,ikiwa tumeamrishwa

kuwa waadilifu mpaka kwa makafiri,basi seuze hawa waislamu wenzetu !

Na pia katika mambo ya sheria za dini hebu tuacheni hamasa,tuangalie maandiko ya dini namna yanavyo tuelekeza.

## Kosa la kumi na sita;

Kisha akasema mbona mko kimya hamkemei ukafiri huu na shirki ya ufalme..!!!

## Jawabu yetu;

Tunavyofahamu sisi kwa mujibu wa mafundisho sahihi ya kiislamu kupitia Qur'an na Sunna za Mtume {s.a.w.} ni kwamba ufalme siyo shirki.

Bali inategemea na matendo ya mfalme mwenyewe kama akiwa muadilifu na kuisimamisha sheria ya Allah {s.a.w.}na kuwafanyia wema raia wake, sheria itampongeza na atalipwa kheri mbele ya Allah {s.a.w.} na atafinikwa na kivuli cha ar'shi ya mwenyezi mungu katika siku ambayo hakuna kivuli isipokuwa kivuli chake.

Na akiwa muovu sheria itamlaumu na atekwenda kuulizwa mbele ya Allah {s.a.w.} na atastahiki adhabu kali kwa khiyana aliyoifanya.

Na ama sisi kama raia wakiislamu tunapo tawaliwa na watawala waovu,inatakikana tuwe hivi;

1-Tuamini kwamba hiyo ni adhabu ya mwenyezi mungu kwetu sisi kutokana maovu yetu,kwahiyo wajibu ni kutubia na kuacha dhambi zetu.

2-Kufanya subra,na kuwaombea dua njema za siri na dhahiri, mwenyezi mungu awaongoze kwenye kheri, na awajaalie uislamu

upate nguvu kupitia mikono yao,na awape nyoyo za huruma kwa raia wao, na kama watawala hao ni waislamu, basi ni kumuomba Allah tukinge na shari zao.

3- kuwatii katika mambo ambayo si ya kumuasi Allah {s.a.w.}.

4- kuwapa nasaha za siri wanapo kosea kwa wale walio na uwezo wa kufanya hivyo,na si kupambana nao juu ya vinara,na kama mtawala ni muovu basi kumwambia ukweli mbele yake na hali yeye yupo hapo hapo,na kufanya hivyo ni jihadi bora.

Ama kuwatukana juu ya vinara,na kuwahamasisha watu kufanya uasi,hizo ni sera potofu za hamasa za kikhawaariji ambazo ziko mbali na mafundisho ya kiislamu.

Haya na mengine mengi ambayo siku yataja,ndiyo ninayo yafahamu mimi kwa mujibu wa mafundisho sahihi ya Sunna sahihi za Mtume Muhammad {s.a.w.},na maneno ya maulamaa wakubwa wa Ah'lus Sunnati wal Jamaa.

Ama wewe kwa mujibu wa msimamo wako huo potofu wa kwamba ufalme ni shirki, na ni ukafiri utalazimika kuzijibu hoja zote tulizozitoa tena kielimu,na si kwa hamasa za wanasiasa.

Kwasababu wanasiasa wengi ni warongo,na wanawatumia waislamu kama ngazi tu, ili kufikia mas'lahi yao,na kuna wengi wao pia ni majahili hawayajui mafundisho sahihi ya uislamu.

Lakini pamoja na ujahili wao huo wao ndio wasemaji wakuu wa waislamu ! na ninatarajia kuandika makala maalumu kuhusu mas'ala haya -Inshaallah-.

Na ama haya makosa kumi na sita tuliyo yataja hapa ni machache katika makosa mengi ya kielimu yaliyo jaa katika makala hiyo yenye kurasa nne tu !

na kuna mengi tumeyawacha ili kufupisha.

فسل ذا خبرة ينبيك عنهم
لتعلم كم خبايا فى الزوايا

## KHATIMA

Mwisho kabisa nina muomba Sheikh wa msikiti wa kwa mnyamani Buguruni-Dar es salaam na vijana wake walio msaidia kuitawanya makala hiyo waisome makala hii kwa makini na utulivu,na kama wanalo lolote lile la kujibu basi wajitahidi sana yawe ni majibu ya kielimu.

Na kujiepusha na lugha za matusi ili waislamu wapate faida,hali wakijua kwamba nasisi tuko tayari katika kupambana na upotoshaji wowote ule kwa hali na mali,na mategemeo yetu katika hili ni Allah {s.w.t.}.

Na tuna muomba mwenyezi mungu aijaalie makala hii iwe ni yenye baraka yenye kuwanufaisha waislamu,na yoyote anaye kusudia kuijibu kwa ajili ya kutaka kupotosha haqi.

Yaa Rabbi tukinge na shari yake,na ujaalie upotoshaji huo ni maangamivu juu yake,Ewe mola wetu tujaalie Ikh’lasi katika kauli zetu,na matendo yetu ya dhahiri,na ya siri.

Aamiin,Aamiin.

Nyuma ya makala hii tumeiambatanisha hiyo makala ya sheikh wa msikiti wa Buguruni kwa mnyamani,ambayo imejaa upotoshaji, tumefanya hivyo ili ujionee mwenyewe.

**Fuatilia mfululizo wa makala zetu;**

HII NDIYO DAAWA YETU JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIH

- **1,2,3.) Athari mbaya ya Uzushi katika uislamu.**

- **4,)Uharamu wa kuyajengea makaburi**

- **5)Uharamu wa kuyajengea makaburi.**
  **Majibu na maelezo**

- **6)Uharamu wa kuswali kuelekea makaburi.**

Ndiyo hii iliyoko mikononi mwako .

Tanbihi;

1-Tafadhali usikose makala ifuatayo ni muhimu.

2 -Ukiipata makala hii toa copy nyingine na umpe mwenzako kwa lengo la kueneza ujumbe.

**وصلى الله وسلم وبارك على محمد وعلى آله وصحبه أجمعين.**
**وآخر دعوانا أن الحمد لله رب العالمين.**